



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

MIKUTANO YA KUKUSANYA MAONI KUHUSU VIWANGO VYA NAULI ZA TRENI KWA
MIKOA YA DAR ES SALAAM, KIGOMA NA MWANZA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imepokea maombi kutoka Shirika la Reli Tanzania (TRC) ikiomba ongezeko la nauli kwa asilimia 15 kwa abiria wanaotumia usafiri wa treni Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria Na. 3 ya LATRA, 2019 Mamlaka inapaswa kukusanya maoni ya wadau kabla ya kufikia uamuzi wa kuridhia viwango vya nauli kwa huduma zinazodhibitiwa na Mamlaka ikiwemo nauli za treni.

Katika kulitekeleza hilo, Mamlaka imeandaa mkutano wa kupokea maoni ya wadau wa usafirishaji, ikiwa ni pamoja na watoa huduma, watumiaji wa huduma na wananchi kwa ujumla. Mikutano hiyo itafanyika **tarehe 19, 22 na 24 Agosti 2022 saa nne kamili asubuhi (4:00)**, kwa Dar es salaam (Ukumbi wa Anatorglo), Kigoma (Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa) na Mwanza (Ukumbi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa) mtawalia.


Nauli zinazopendekezwa na TRC ni Kama ifuatavyo:

Jedwali Na. 1. Nauli za treni ya abiria ya 'Deluxe' kutoka Dar es salaam							
Vituo	Daraja la pili-kulala			Daraja la pili-kukaa		Daraja la tatu	
	Km	Nauli ya zamani	Nauli Pendekezwa	Nauli ya zamani	Nauli Pendekezwa	Nauli ya zamani	Nauli Pendekezwa
Ruvu	79	13,800	15,800	8,300	9,500	5,800	6,700
Wami	151	18,000	20,700	10,800	12,400	7,600	8,700
Morogoro	202	21,200	24,300	12,700	14,600	8,900	10,300
Mkalamo	203	21,200	24,300	12,700	14,600	8,900	10,300
Kilosa	289	25,400	29,200	15,300	17,500	10,700	12,300
Korogwe	291	25,400	29,200	15,300	17,500	10,700	12,300
Mombo	335	27,500	31,600	16,500	19,000	11,600	13,300
Dodoma	465	34,900	40,100	21,000	24,100	14,700	16,900
Same	459	33,800	38,900	20,300	23,400	14,200	16,400
Moshi	558	39,100	45,000	23,500	27,000	16,500	18,900
Arusha	644	44,400	51,000	26,700	30,600	18,700	21,500
Tabora	850	54,900	63,200	33,000	37,900	23,100	26,600
Urambo	940	59,200	68,000	35,500	40,800	24,900	28,600
Kigoma	1,254	76,100	87,500	45,700	52,500	32,000	36,800

Jedwali Na. 2. Nauli za treni ya abiria daraja kawaida kutoka Dar es salaam							
Vituo	Umbali KM	Daraja la Kwanza		Daraja la Pili		Daraja la Tatu	
		Nauli ya zamani	Nauli Pendekezwa	Nauli zamani	Nauli Pendekezwa	Nauli zamani	Nauli Pendekezwa
Pugu	20	12,200	14,000	10,600	12,100	6,100	7,000
Ngerengere	144	20,700	23,800	16,600	19,100	9,000	10,300
Morogoro	202	24,300	28,000	19,200	22,000	10,200	11,800
Kimamba	271	28,000	32,200	21,700	25,000	11,500	13,200
Kilosa	289	29,200	33,600	22,600	26,000	11,900	13,700
Dodoma	465	40,100	46,100	30,300	34,900	15,600	18,000
Manyoni	595	47,400	54,500	35,500	40,800	18,100	20,800
Itigi	635	49,800	57,300	37,200	42,800	18,900	21,800
Tabora	850	63,200	72,600	46,700	53,700	23,500	27,000
Kaliua	973	70,500	81,000	51,800	59,600	26,000	29,900
Isaka	982	71,700	82,400	52,700	60,600	26,400	30,300
Uvinza	1,141	81,400	93,600	59,600	68,500	29,700	34,100
Shinyanga	1,045	75,300	86,600	55,300	63,600	27,600	31,800
Mto Ugalla	1,083	77,700	89,400	57,000	65,500	28,500	32,700
Katumba	1,149	81,400	93,600	59,600	68,500	29,700	34,100
Mpanda	1,183	83,800	96,400	61,300	70,500	30,500	35,100
Mwanza	1,229	86,200	99,200	63,000	72,500	31,400	36,000
Kigoma	1,254	87,500	100,600	63,900	73,500	31,800	36,500
Nauli zinazopendekezwa zitawasilishwa kwa ufafanuzi zaidi wakati wa mkutano husika							

Kutokana na umuhimu wa mkutano huo, LATRA inawaalika wadau wa sekta ya reli na wananchi kwa ujumla kushiriki bila kukosa katika mkutano kama ilivyoelezwa hapo juu. LATRA pia itapokea maoni kwa maandishi. Maoni hayo yawasilishwe katika Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu, S.L.P. 3093, Dar es Salaam, iliyopo katika Jengo la Mamlaka, Barabara ya Nkrumah kabla ya tarehe 31 Agosti, 2022. Aidha, maoni ya wadau yanaweza kutumwa kwa barua pepe kupitia anuani hizi: info@latra.go.tz na dg@latra.go.tz.

Imetolewa na:



J. J. Kahatano

Kny: Mkurugenzi Mkuu,
9 Agosti, 2022

